

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA

SHULE YA SEKONDARI MCHOMBE,

S. L. P. 04,

IFAKARA.

TAREHE.....

Kumb. MSS/MLB/E/SEC/2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

## 1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari mchombe mwaka 2021. Shule itafunguliwa tarehe..... Unapaswa kufika shuleni siku hiyo saa1:00 asubuhi bila kukosa.

**NB: Kuchelewa kuripoti au kutoripoti kwa makusudi, hatua za kisheria zitachukuliwa juu ya mzazi na mwanafunzi.**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

#### A: Sare ya wavulana:

- i. Sururali 2 za rangi ya damu ya mzee.
  - Ziwe na malinda(celebration), isiyo na malinda haitakubalika
  - Zisiwe suruali za kubana, ziwe suruali za hesima.
  - Ziwe na mifuko mitatu, mbele 2 na nyuma 1.(Mifuko isiwe ya kubandika)
- ii. Mashati 2 meupe (tetroni), mikono mifupi. Yasiwe ya kubana na yasiwe madogo.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na kamba(gidamu) jozi 2. Mabuti, Raba, Viatu vyenye visigino virefu na viatu visivyo na kamba havitakubalika.
- iv. Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote jozi 2.
- v. Mkanda wa ngozi mweusi.

#### B: Sare ya wasichana:

- i. Sketi 2 za rangi ya damu ya mzee (Mshono ni malinda)
  - Sketi ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu kutoka kwenye unyayo. Sketi fupi hazitakubalika
  - Nusu kanzu na hijabu zinaruhusiwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa na shule.
- ii. Mashati 2 meupe (tetroni), mikono mifupi. Yasiwe ya kubana na yasiwe madogo.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na kamba(gidamu) jozi 2. Mabuti, Raba, Viatu vyenye visigino virefu na viatu visivyo na kamba havitakubalika.
- iv. Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote jozi 2.

### **C: Sare za michezo:**

Sare ya michezo ni T-shirt yenye rangi ya kijani pamoja na bukta yenye rangi ya kijani kwa wavulana na kwa wasichana ni T-shirt yenye rangi ya kijani na tracksuit ya kijani.

### **2.2 Vifaa vya masomo:**

- Unatakiwa kuja na daftari kubwa 11 (11 Counterbooks), kalamu na mkebe wa hesabu
- Daftari 09 kwa ajili ya majaribio

### **2.3 Vifaa vya usafi:**

- Wavulana waje na jembe moja na fagio la chelewa
- Wasichana waje na kwanja na fagio la chelewa

**NB: Njoo na kifaa cha usafi pesa haitapokelewa**

## **3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule ya sekondari mchombe inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu **na. 25** ya mwaka **1978**, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu yenye dhamana ya elimu nchini na **Ofisi ya Rais-TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Uwapo hapa shuleni, utatakiwa kuzingatia yafuatayo;

- i. Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- iii. Ni lazima kujisomea wakati wa usiku uwapo shuleni au hata nyumbani.
- iv. Ni lazima kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine unazopewa.
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya miapaka hiyowakati wote ukiwa mwanafunzi katika shule hii.
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufnya hivyo.
- viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- ix. Kutunza mali ya umma

### **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- i. Wizi
- ii. Uasherati
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, kokeini, mirungi, ugoro, kuberi n.k
- v. Kupigana au kupiga

- vi. Kudharau bendera ya Taifa
- vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- viii. Kupata mimba ( kuwa mjamzito)
- ix. Kutoa mimba
- x. Kuoja au kuolewa
- xi. Kumiliki au kuwa na simu ya mkononi shuleni
- xii. Kukaa kwenye vijiwe, geto au kukutwa katika nyumba za starehe (Rest Houses & Bar)
- xiii. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kwa namna yoyote katika kuvuruga amani na usalama wa shule.

NB: Iwapo mwanafunzi amepata shule binafsi, tafadhali toa taarifa ya maandishi kwa mkuu wa shule mapema.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MCHOMBE**

.....

GOOD M. CHAMI

MKUU WA SHULE

0783459127/ 0674724769/ 0655847931